

Ruwaza Zinazojitokeza kwenye Sinonimu za Mkopo katika Lugha ya Kiswahili

*George Jerald Kitundu*¹
Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Saalam
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.1>

Ikisiri

Kila lugha hukopa maneno kutoka lugha ngeni moja au zaidi kila zinapotagusana na jamiilugha ngeni. Kwa hiyo, suala la ukopaji wa maneno si la lugha fulani mahususi bali ni la lugha zote. Lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha zingine, imekopa maneno kutoka lugha za kigeni kama Kiingereza, Kiarabu na Kireno. Ukopaji maneno katika lugha hutokana na sababu mbalimbali mojawapo ikiwa ni kasumba ya wazungumzaji kukopa maneno kutoka lugha za kigeni hata kama msamiati unaokopwa upo katika lugha husika au ulikwisha kukopwa kutoka lugha za kigeni (Kiango, 1999). Matokeo ya ukopaji huo ambao unatokana na kasumba, ni kuwa na maneno mawili au zaidi ya kigeni yanayorejelea dhana ileile. Kuwapo kwa maneno mawili au zaidi yanayorejelea dhana ileile katika lugha huibua sinonimu. Wataalamu kama Ullmann (1967) na Kitundu (2022) wanadai kuwa sinonimu katika lugha hazijakaa kivoloya bali hufuata ruwaza fulani kimatumizi. Lugha ya Kiswahili kama tulivyoeleza ina maneno mengi ya mkopo kutoka lugha za kigeni zaidi ya 13. Hivyo, upo uwezekano wa kuwa na maneno mawili au zaidi kutoka lugha ngeni mbili au zaidi yanayoelezea dhana ileile. Hata hivyo, suala hili bado si bayana katika lugha hii. Kwa hiyo, ipo haja ya kuchunguza zaidi suala hili. Kwa mantiki hiyo, makala haya yanachunguza ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo katika Kiswahili. Ili kufikia azma hiyo, data za makala haya zimekusanywa kutoka katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2019) kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini na kutoka kwa watoataarifa kwa kutumia mbinu ya hojaji. Ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Vijenzi Semantiki pamoja na Nadharia ya Matumizi.

1.0 Utangulizi

Kiswahili ni moja ya lugha zenye maneno ya mkopo kutoka lugha mbalimbali za kigeni. Maneno hayo yameingia katika Kiswahili kutokana na shughuli za biashara, elimu, siasa, utawala na masuala mbalimbali kama ndoa. Kutokana na kuwapo kwa maneno ya mkopo na yale ya asili, msamiati wa Kiswahili unaweza kuwekwa katika makundi makubwa mawili. Kwanza, ni msamiati wa asili ambao hautokani na ukopaji, na pili, ni msamiati wa mkopo ambao unatokana na kukopa kutoka

¹ Barua pepe: george.kitundu@duce.ac.tz

lugha za kigeni kama Kiingereza, Kigiriki, Kiajemi, Kifaransa na Kireno (Kiango, 1999). Kamusi ya TUKI (2019) inaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imekopa msamiati kutoka lugha za kigeni zaidi ya 13. Wazungumzaji wa lugha wana kasumba ya kukopa msamiati kutoka lugha za kigeni kila wanapotagusana na jamii hizo hata kama msamiati unaoelezea dhana hiyo ulikwisha kukopwa kutoka lugha zingine. Hali hii, hapana shaka, imeongeza msamiati wa mkopo katika Kiswahili, jambo ambalo si ajabu kukuta maneno mawili au zaidi kutoka lugha ngeni mbili au zaidi huelezea dhana ileile. Kuwapo kwa maneno mawili au zaidi kutoka lugha ngeni mbili au zaidi yanayorejelea dhana ileile husababisha kuibuka kwa sinonimu zinazohusisha maneno yote ya kigeni. Sinonimu katika lugha zina namna yake ya matumizi katika miktadha mbalimbali. Hali hii huibua ruwaza mbalimbali za sinonimu. Makala haya yanaangazia ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo katika lugha ya Kiswahili. Katika kuangaza huko, kwanza makala yametoa utangulizi wa jumla kisha kufuatiwa na ufafanuzi wa dhana za msingi kama sinonimu, utohozi na ruwaza. Baada ya ufafanuzi huo, makala yamebainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika makala haya kisha kueleza nadharia zilizoongoza makala haya. Baada ya maelezo hayo, makala yamebainisha ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu zinazohusisha maneno ya mkopo tu katika lugha ya Kiswahili. Mwisho wa makala haya limetolewa hitimisho la jumla.

2.0 Dhana ya Ukopaji wa Maneno katika Lugha

Ukopaji wa maneno katika lugha ni uchukuaji au uhamishaji wa maneno kutoka lugha zingine na kuwa sehemu ya msamiati wa lugha pokezi (Kiango, 1999; Matinde, 2012). Kila lugha hukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali. Kwa hiyo, ukopaji wa maneno ni jambo la kawaida katika lugha. Haya yanaelezwa pia na Kiango (1999) na King'ei (2010) kuwa ukopaji wa maneno si suala la lugha fulani maalumu tu, bali ni mbinu ya kukuza lugha inayotumiwa na lugha zote duniani. Maneno yanaweza kukopwa kutoka lugha ambazo kiisimu ziko katika familia moja au kutoka lugha za kigeni ambazo zinatofautiana kiisimu. Maneno yanayokopwa yanaweza kubadilishwa kifonolojia, kimofolojia au kisemantiki ili yawe na tabia sawa na maneno ya lugha pokezi au kuyachukua kama yalivyo kutoka lugha chanzi na kuyatumia katika lugha pokezi (Kiango, 1999; Hoffer, 2005; Shembilu, 2020).

Maneno hukopwa katika lugha kutokana na sababu mbalimbali. Mosi, ni mahitaji ya msamiati katika lugha kwa ajili ya kuelezea dhana au kitu ambacho hakikuwa kinajulikana katika jamii ya lugha hiyo. Pili, ukopaji unaweza kutokana na mwingiliano wa nguvu za kisiasa ambazo husababisha pia jamii kutumia maneno ya lugha tawala, na hivyo, kuongeza msamiati katika lugha lengwa (Robins, 1980; Chuwa, 1988). Tatu, msamiati katika lugha hukopwa kutokana na kasumba ya wazungumzaji fulani wanaopenda kukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali pindi kunapokuwa na mtagusano wa jamii yao na jamii nyingine ya kigeni licha ya kuwapo kwa msamiati unaorejelea dhana zinazokopwa (Kiango, 1999; Matinde,

2012). Ukopaji huu unaotokana na kasumba ya wazungumzaji kwa kiasi kikubwa ndio unaosababisha kuwe na maneno mawili au zaidi kutoka lugha ngeni mbili au zaidi. Hali hiyo husababisha kuibuka kwa maneno mawili au zaidi yenye maana sawa, yaani sinonimu. Hivyo, hii ndio sababu makala haya kuchunguza sinonimu zinazotokana na maneno ya mkopo tu katika lugha ya Kiswahili.

Kama ilivyoielezwa awali, Kiswahili ni moja ya lugha zenye maneno ya mkopo kutokana na kuwapo kwa mtagusano na jamii mbalimbali za kigeni kama Kireno, Kiarabu, Kiingereza, Kihindi, Kituruki na Kijerumani (Chuwa, 1988; Beshu, 1995; Chacha na Malangwa, 2019). Kutokana na mtagusano huo, wazungumzaji wa lugha hapo awali walikopa msamiati kila walipotagusana na jamii ngeni hata kama msamiati ulioelezea dhana fulani walikwisha kukopa kutoka lugha zingine za kigeni (Mohamed, 2010; Zhou, 2016; Kitundu, 2022). Maelezo hayo yana maana kuwa wazungumzaji walipotagusana na Wajerumani walikopa baadhi ya msamiati wa dhana fulani kama *shule* kisha walipotagusana tena na jamii nyingine kama Waingereza walikopa pia msamiati *skuli* ambao unarejelea dhana ileile. Matokeo ya hali hii ni kuwa na maneno mengi kutoka lugha mbalimbali yanayorejelea dhana ileile, jambo ambalo husababisha kuibuka kwa sinonimu zinazotoka katika lugha mbalimbali za kigeni. Sinonimu hizo ndizo zinazoitwa sinonimu za mkopo katika lugha. Jambo hili ndilo linalochunguzwa katika makala haya ili kubaini sinonimu zinazotokana na ukopaji tu pamoja na ruwaza zake. Ufafanuzi zaidi kuhusu sinonimu unatolewa katika kipengele kinachofuata.

2.1 Dhana ya Sinonimu

Sinonimu ni dhana iliyofasiliwa na wataalamu mbalimbali. Chacha na Malangwa (2019) wanaeleza kuwa sinonimu ni maneno yenye maumbo tofauti lakini yana maana moja inayofanana au inayokaribiana. Naye Kahigi (2019) anaeleza kuwa sinonimu ni maneno mawili au zaidi yenye maumbo tofauti lakini yana maana ileile au inayokaribiana. Fasili za wataalamu hao zinaonesha kuwa sinonimu zinaweza kuwa na maana sawa au maana zake zinakaribiana. Hali hii inatupatia makundi mawili ya sinonimi: sinonimu kamili na zisizo kamili (Ndimele, 1997). Sinonimu kamili ni zile ambazo zinafanana katika miktadha yote ya kimatumizi na zina athari sawa katika kila miktadha. Sinonimu zisizo kamili ni zile ambazo zinafanana katika baadhi ya virejelewa huku virejelewa vingine vikifanana na virejelewa vya maneno mengine. Ingawa husemwa kuwa sinonimu kamili ni chache lakini ukweli ni kwamba zipo. Baadhi ya mifano ya sinonimu kamili ni pamoja na sarufi maana/semantiki, nazali/king'ong'o (Ullmann, 1967; Ndimele, 1997; Resani, 2015; Kahigi, 2019). Pamoja na aina hizo, Kitundu (2022) anaeleza kuwa kutokana na ukopaji wa maneno, sinonimu katika lugha zinaweza kuwekwa katika makundi matatu. Kwanza, ni sinonimu za asili tu. Hizi ni zile ambazo hazihusishi neno la mkopo katika seti moja ya sinonimu. Pili, kuna sinonimu za mkopo tu. Kundi hili la sinonimu halihusishi neno la asili, na tatu ni sinonimu za asili na za mkopo, yaani zile zinazohusisha neno moja la asili na lingine/mengine ni ya mkopo. Makala haya

yanachunguza sinonimu za mkopo tu ili kuona ruwaza zake. Kipengele kinachofuata kinafafanua ruwaza za sinonimu.

2.2 Ruwaza za Sinonimu

Neno ruwaza limefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalani, Massamba (2009) anaeleza kuwa ruwaza ni utaratibu wa kimpangilio wa vipashio vya lugha. Kwa hiyo, vipashio vya lugha kama maneno huweza kupangwa katika mfuatano fulani kulingana na sifa au tabia zake. Pia, TUKI (2019) inafafanua kwamba ruwaza ni mpangilio maalumu wa mambo. Mpangilio huo unahusisha uwekaji wa vitu katika mfuatano fulani kulingana na sifa au vigezo mbalimbali. Maelezo ya Massamba (2009) na TUKI (2019) yana maana kuwa vipashio vya lugha, maneno yakiwamo, havipangwi kiholela tu, bali hufuata misingi au kanuni fulani. Kanuni hizo zinatupa neno au kipashio cha kwanza, cha pili, cha tatu na kuendelea. Sinonimu zinaweza kupangwa katika mfuatano kwa kuzingatia vigezo mbalimbali, kimojawapo kikiwa ni namna maneno hayo yanavyotumika katika jamii. Kwa hiyo, dhana ya ruwaza za sinonimu katika makala haya inatumiwa kama mpangilio wa sinonimu kulingana na matumizi yake katika jamii. Kigezo kikuu kinachotumika kupanga maneno yenye sifa ya usinonimu ni matumizi yake katika jamii, yaani namna watu wanavyoyatumia au wanavyoyafahamu maneno katika seti moja ya sinonimu. Hali hii ya matumizi husababisha kuwa na neno la kwanza ambalo lina matumizi makubwa kisha likifuatiwa na neno la pili, la tatu au la nne. Hali hii huibua ruwaza za sinonimu.

Suala la ruwaza za sinonimu limejadiliwa na watafiti mbalimbali. Ullmann (1967), Palmer (1976), Kreidler (1998) na Danglli (2010) wanadai kuwa lugha ya Kiingereza imekopa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni kama Kigiriki na Kifaransa. Kuingia kwa maneno ya mkopo katika lugha hiyo kulisababisha kuibuka kwa ruwaza za sinonimu zinazohusisha maneno ya asili na yale ya mkopo kutoka lugha ngeni moja au zaidi. Ruwaza hizo ni za uwili na utatu. Katika ruwaza hizo, Ullmann anadai kuwa maneno ya asili ndiyo yanayokuwa ya kwanza katika ruwaza kwa sababu yanatumika zaidi kuliko yale ya kigeni. Maneno ya kigeni yanafuatia yale ya asili kimatumizi. Hivyo, yanakuwa ya pili na ya tatu. Hata hivyo, anadai kuwa ruwaza hizo hubadilika kutoka muktadha mmoja hadi mwingine. Lugha zingine ambazo zimebainika kuwa na ruwaza za sinonimu kutokana na kuwapo kwa maneno ya mkopo na ya asili ni Kifaransa na Kialbania ambazo ruwaza zake zinafanana kwa kiasi kikubwa na zile za Kiingereza (Ullmann, 1967; Danglli, 2010).

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, Kitundu (2022) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza za sinonimu zinazohusisha neno la asili na lingine la mkopo kutoka lugha moja au zaidi. Anabainisha ruwaza nne za sinonimu zinazojitokeza katika lugha hiyo. Ruwaza hizo ni za uwili, utatu, unne na utano. Kati ya ruwaza

hizo, Kitundu anadai kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiswahili, yaani yasiyotokana na ukopaji ndiyo yanayotumika zaidi yakifuatiwa na yale ya Kiswahili yenye asili ya kigeni. Hata hivyo, kama ilivyo kwa Ullmann katika lugha ya Kiingereza, naye anadai kuwa ruwaza zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili hubadilika kulingana na mabadiliko ya matumizi katika miktadha mbalimbali.

Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu mbalimbali yanaonesha kuwa lugha inapokuwa na maneno ya asili na ya mkopo kuna sinonimu zinazojitokeza. Sinonimu hizo huibua ruwaza mbalimbali. Wataalamu tangulizi kama Ullmann (1967), Kreidler (1998), Danglli (2010) na Kitundu (2022) walichunguza zaidi kuhusu ruwaza za sinonimu zinazohusisha maneno ya asili na ya mkopo. Lugha ya Kiswahili kama ilivyoelezwa hapo awali imekopa maneno kutoka lugha za kigeni zaidi ya 13 kama zinavyobainika katika kamusi ya TUKI (2019). Kutokana na idadi hiyo ya lugha pamoja na kasumba ya wazungumzaji kukopa maneno hata kama yapo au yalikuwisha kukopwa, hapana shaka kuwa kuna uwezekano wa kuwapo kwa maneno mawili au zaidi yanayorejelea dhana moja kutoka lugha ngeni mbili au zaidi, hivyo, kuibua ruwaza za sinonimu za mkopo. Kwa mantiki hiyo, ipo haja ya kuchunguza zaidi suala la ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo katika Kiswahili. Katika uchunguzi huo dhana ya ruwaza inatazamwa katika vipengele viwili. Mosi, ni idadi ya ruwaza ambayo inapatikana kwa kuangalia idadi ya maneno katika seti moja ya sinonimu. Seti ya sinonimu yenye maneno mawili inajenga ruwaza moja ya uwili na yenye maneno matatu inajenga ruwaza ya utatu.

Pili, ruwaza zinatazamwa katika mpangilio au mfuatano wa maneno katika seti ya sinonimu. Katika mpangilio wa maneno kinachochunguzwa ni namna maneno katika seti moja ya sinonimu yanavyotumika. Resani (2015), Chacha na Malangwa (2019), Kahigi (2020) na Kitundu (2022) wanadai kuwa lugha inapokuwa na sinonimu, kuna tofauti za kimatumizi zinazojitokeza. Tofauti hizo zinajitokeza katika urasmi na usirasmi, vidokezo hasi au chanya, au ukali na ulaini. Hali hii ya matumizi huibua neno moja katika seti ya sinonimu kuwa na matumizi zaidi au matumizi fulani kuliko mengine. Kuwapo kwa matumizi makubwa ya neno moja kuliko lingine katika seti ya sinonimu ndiko kunakoibua ruwaza za sinonimu katika lugha. Kipengele kinachofuata kinafafanua mbinu za utafiti zilizotumika katika makala haya.

3.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya umetumia mbinu kadha wa kadha katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Utafiti huu umefanyika mkoani Dar es Salaam, hususani katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika chuo hicho, data zimekusanywa katika Makavazi ya TATAKI na kutoka kwa watoataarifa 60. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni uchambuzi wa matini ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) (2019) pamoja na hojaji na usaili kutoka kwa watoataarifa 30. Watoataarifa hao walipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ambapo

kulikuwa na matabaka mawili ya wanafunzi wanaosoma shahada ya awali na shahada ya umahiri. Kila kundi lilikuwa na watoataarifa 15 ambao walichaguliwa kinasibu kwa kugawa hojaji kuanzia mtu wa kwanza hadi wa 15. Waliopata hojaji ndio waliokuwa sampuli ya watoataarifa. Kwa kiasi kikubwa data za makala haya ni zile zinazohusisha sinonimu za mkopo tu, yaani zisizo na neno la asili katika seti ya sinonimu. Data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui kwa sababu zimewekwa katika makundi kulingana na idadi ya seti za sinonimu pamoja na lugha zinazohusika. Seti za sinonimu zinazohusisha maneno mawili kutoka lugha mbili tofauti zimewekwa katika kundi lake kisha zile zinazohusisha maneno matatu zimewekwa pia katika kundi lake na kuendelea. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Vijenzi Semantiki ambayo ilitumika kubainisha maneno yenye kufanana kimaana kisha Nadharia ya Matumizi ilitumika kuchunguza namna maneno yanavyotumika katika jamii ili kubaini neno lenye matumizi makubwa kuliko lingine. Maneno yaliyobainishwa kuwa yanatumika zaidi katika jamii kwa ujumla kuliko mengine ndiyo yaliyowekwa mwanzoni mwa ruwaza. Pamoja na mbinu hiyo ya uchambuzi wa data, makala haya pia yametumia mbinu ya ufafanuzi. Kipengele kinachofuata kinabainisha nadharia zilizoongoza utafiti huu.

4.0 Nadharia za Utafiti

Makala haya yameongozwa na nadharia mbili, yaani Nadharia ya Vijenzi Semantiki na Nadharia ya Matumizi. Nadharia hii inaegemea katika msingi kuwa maneno yanajengwa na vijenzi fulani ambavyo vinaweza kubainishwa, na hivyo, kuelezea kila neno. Vijenzi hivyo vinabainishwa na Weisgerber kuwa ni jenda au koo (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019). Vijenzi vya kila neno ndivyo vinavyojenga maana ya jumla ya kila neno na vijenzi hivyo ndivyo hutofautisha au kuonesha uhusiano uliopo baina ya maneno yaliyo katika kikoa kimoja. Kwa ajili ya kupata mwanga zaidi kuhusu nadharia hii, tutazame mfano wa kikoa cha maana cha samani katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Kikoa cha Maana cha Samani

Kategoria ya Samani	Vijenzi Maana			
	Kiegemeo cha Nyuma	Yenye Miguu	Sehemu ya Kukalia	Enye Vishikio
<i>kiti</i>	+	+	+	-
<i>sofa</i>	+	+	+	+
<i>kigoda</i>	-	+	+	-

Chanzo: Kahigi (2019)

Katika Jedwali Na. 1 tunaona kuwa *kiti* cha kawaida hakina vishikio huku *kigoda* kikiwa hakina kiegemeo cha nyuma na vishikio (Kahigi, 2019). Katika mfano huo, maana ya kiti ni kifaa kilichotengenezwa kwa ajili ya kukalia na ambacho kina egemeo kwa nyuma na miguu. Mfano huu wa kikoa pia unadhihirisha kuwa

maneno yanayojenga kiko maana cha samani kama *kiti*, *sofa* na *kigoda* yana sifa ya usinonimu. Hii ni kwa sababu maneno hayo yanafanana katika baadhi ya vijenzi maana vyake hususani dhana ya kuwa na *miguu* na *sehemu ya kukalia*. Kwa hiyo, Nadharia ya Vijenzi Semantiki imetumika kubainisha maneno yenye maana zinazofanana au kukaribiana, yaani sinonimu kutoka katika kamusi teule kwa kuangalia mfanano wa vijenzi semantiki vya maneno husika. Mtafiti, kwanza alibainisha vijenzi semantiki vyote kwa kila neno kisha kulinganisha ili kuona mfanano wake.

Kama ilivyotajwa awali, Nadharia ya Matumizi iliyoasisiwa na Wittgenstein (1953) imetumika pia. Wittgenstein anadai kuwa maana ya neno ni matumizi yake katika lugha. Anaendelea kudai kuwa mtu hapaswi kuuliza maana ya neno bali aulize matumizi ya neno. Hii ni kwa sababu kila neno la lugha lina kazi yake, hivyo, mtu akitaka kung'amua maana yake basi aangalie namna neno hilo linavyotumika katika jamii (Chacha na Malangwa, 2019). Mawazo ya nadharia hii ya kuzingatia muktadha katika kufikia mahitimisho ya neno ndiyo yaliyotungoza kuchunguza namna maneno yanavyotumika katika jamii kisha kupata neno linalotumika na lisilotumika. Neno linalotumika sana ndilo linalokuwa la kwanza katika ruwaza kisha linafuatiwa na lile ambalo halitumiki sana katika seti ya sinonimu. Suala hili la uzingativu wa muktadha katika kufikia mahitimisho linaelezwa zaidi na Celeghin (2013) anayedai kuwa tunapochunguza sinonimu, muktadha una nafasi kubwa ya kufikia mahitimisho yetu kuhusu sinonimu. Kwa hiyo, ni muhimu kuhusisha muktadha katika kuchunguza sinonimu na ndiyo maana kiunzi hiki cha kinadharia kimetumika kama mwongozo wa kuchambulia data za utafiti huu. Kipengele kinachofuata kinafafanua ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo katika Kiswahili.

5.0 Ruwaza Zinazojitokeza kwenye Sinonimu za Mkopo katika Kiswahili

Kulingana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo. Ruwaza zilizobainika ni mbili: ruwaza ya uwili na ruwaza ya utatu. Kuwapo kwa ruwaza hizi kunatokana na lugha ya Kiswahili kukopa maneno kutoka lugha za kigeni ambazo katika kamusi ya TUKI (2019) zipo lugha zaidi ya 13 zikiwamo lugha ya Kiingereza, Kihindi, Kihispaniola, Kiajemi, Kiarabu, Kireno na Kijerumani. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa wazungumzaji wa lugha, Kiswahili kikiwamo, wana tabia ya kukopa msamiati kila wanapokutana na wazungumzaji wa lugha nyingine. Kwa hiyo, katika Kiswahili maneno yamekuwa yakikopwa hata kama neno linaloelezea dhana hiyo lilikwisha kukopwa kutoka lugha nyingine. Hali hii ndiyo iliyosababisha kuibuka kwa maneno mawili au zaidi kutoka lugha mbili na zaidi za kigeni yanayorejelea dhana ileile. Hali hii imeibua sinonimu za mkopo katika Kiswahili. Ufafanuzi wa ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo unatolewa katika vipengele vinavyofuata. Katika ufafanuzi huo, maoni ya

watoataarifa walio wengi ndiyo yaliyotumika kuhitimisha matumizi ya neno moja linapolinganishwa na neno lingine lenye maana ileile.

5.1 Ruwaza ya Uwili inayojitokeza kwenye Sinonimu za Mkopo katika Kiswahili

Kulingana na data iliyokusanywa na kuchambuliwa, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayojitokeza kwenye sinonimu za mkopo. Ruwaza ya uwili inahusisha seti za sinonimu zenye maneno mawilimawili kutoka lugha ngeni mbili. Mpangilio wa maneno katika ruwaza hizi unatokana na maoni ya watoataarifa kuhusu maneno yanayotumika zaidi katika seti husika. Kwa hiyo, maneno yenye matumizi makubwa au yanayotumika zaidi ndiyo yaliyokuwa ya kwanza katika ruwaza. Ruwaza ya uwili ina ruwaza ndogondogo ndani yake ambazo zinahusisha seti za sinonimu kutoka lugha tofautitofauti. Ruwaza zilizobainika zinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

5.1.1 Ruwaza ya Kiarabu-Kihindi

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili ya Kiarabu-Kihindi. Ruwaza hii inahusisha neno moja la Kiswahili lenye asili ya Kiarabu na lingine lenye asili ya Kihindi. Kuwapo kwa ruwaza hii kunatokana na kuwapo kwa maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiarabu na ya Kihindi yanayorejelea dhana ileile. Kati ya data zilizokusanywa, imebainika kuwa kuna seti 4 za sinonimu zinazojitokeza. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii tutazame data katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Ruwaza ya Kiarabu-Kihindi

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiarabu	Kihindi	
1.	mbamia	mbinda	+mmea ambao huzaa matunda ambayo yakitiwa maji huteleza kama pombo
2.	amiri	jemadari	+kiongozi mkuu wa jeshi
3.	msafara	charo/kafila	+kikundi cha wasafiri
4.	ada	kodi	+malipo yanayotolewa ili kupata huduma kama vile elimu au tiba

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 2 linaonesha data za utafiti zinazohusu ruwaza ya uwili ya Kiarabu-Kihindi. Katika Jedwali hilo, maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu yapo mwanzoni mwa ruwaza kwa sababu mengi kati ya hayo yalibainishwa na watoataarifa kama maneno yanayotumika zaidi. Mathalani, maneno kama *mbamia*, *amri* na *ada* yanatumika zaidi kuliko visawe vyake vyenye asili ya Kihindi kama *mbinda*, *jemedari* na *kodi*. Hata hivyo, baadhi ya maneno yenye asili ya Kihindi nayo yalibainishwa na watoataarifa kama maneno yanayotumika zaidi kuliko yale yenye asili ya Kiarabu. Mathalani, neno *kodi* katika baadhi ya miktadha linatumika

zaidi kuliko neno *ada*. Kwa mfano, katika mazingira ya eneo la kujifunzia kama shule au chuo, neno *ada* litatumika zaidi ilhali katika maeneno ya kibishara neno *kodi* ndilo litatumika zaidi.

5.1.2 Ruwaza ya Kiingereza-Kiarabu

Hii ni ruwaza ya uwili inayohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na yale yenye asili ya Kiarabu. Kulingana na data za utafiti huu, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina sinonimu zinazotokana na ukopaji wa maneno kutoka Kiingereza na Kiarabu. Ruwaza hii ina jumla ya seti 42 za sinonimu. Maoni ya jumla ya watoataarifa yanaonesha kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiingereza ndiyo yanayotumika zaidi. Hivyo, yanakuwa ya kwanza kisha yanafuatiwa na yale yenye asili ya Kiarabu. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii, tutazame data katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Ruwaza ya Kiingereza-Kiarabu

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Jumuishi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa
	Kiingereza	Kiarabu		
1.	digrii	shahada	+cheti anachopewa mtu baada ya kuhitimu masomo ya chuo kikuu.	
2.	chati	jedwali	+mchoro katika karatasi unaoeleza habari fulani.	
3.	tebo	jedwali	+orodha ya hesabu za kuzidisha	
4.	alfabeti	abjadi/abtathi	+herufi za lugha zilizopangwa kwa utaratibu maalumu kama vile a, b, ch ambazo hutumiwa katika maandishi.	
5.	dispensari	zahanati	+hospitali ndogo	
6.	wiki	juma	+jumla ya siku saba	
7.	sementi	saruji	+udongo laini unaotengenezwa kwa mchanganyiko wa mawe, chokaa, udongo wa mfinyanzi, na hutumika kutengeneza matofali au kujengea nyumba	
8.	rejesta	sajili	+mtindo wa lugha unaotumiwa mahali fulani ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida	
9.	risiti	stakabadhi	+kipande cha karatasi kinachoonisha kupokewa au kutolewa kwa pesa	
10	pauni	ratili	+kipimo cha uzito wa wakia 16 au kilo 0.45	
11	plastiki	sandarusi	+aina ya mfuko wa kubebea vitu	
12	namba	tarakimu	+alama ya hesabu iliyoandikwa kuonesha idadi	
13	altare	madhabahu	+meza ya kutolea sadaka	
14	bili	ankra	+orodha ya vitu vilivyozwa na bei zake.	
15	apostrofi	ritifaa	+alama ya kung'ong'ea kama ng'ombe	
16	asidi	tindikali	+kemikali yenye sifa ya kuunguza.	

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Jumuishi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa
	Kiingereza	Kiarabu		
17	paragrafu	aya	+tungu la maneno katika maandishi linaloeleza wazo kamili	
18	manifesto	ilani	+tangazo la mipango au madhumuni ya chama cha siasa lenye kuelezea msimamo wa chama kuhusu hali fulani.	
19	kontinenti	bara	+pande mojawapo la nchi kavu duniani.	
20	buluu	nili/samawati	+rangi ya samawati.	
21	cheki	hawala	+cheti maalumu cha benki kitumikacho kuidhinisha anayetakiwa kupewa fedha.	
22	chesi	sataranji	+mchezo unaofanana na drafti unaohusisha kete zenye kingi, malkia, askofu, kasri, walinzi, ngome n.k.	
23	chizi	jibini	+chakula kinachotengenezwa kwa maziwa ya kugandishwa.	
24	dabali	maradufu	+mara mbili ya kitu kingine.	
25	propela	rafadha	+panka inayofungwa katika meli ndege au motaboti na hutumiwa kuendesha chombo hicho	
26	divisheni	daraja	kiwango cha kufaulu mitihani, hasa ya sekondari	
27	peninsula	rasi	+sehemu ya nchi iliyozungukwa na bahari isipokuwa sehemu ndogo	
28	edita	mhariri	+mtu anayefanya kazi ya kusoma na kusahihisha miswada kama vile makala	
29	faili	jalada	+jalada la kuwekea barua, nyaraka au karatasi kwa kufuata utaratibu fulani	
30	fanicha	samani	+vyombo vya nyumbani kama vile meza, viti, kabati au kitanda	
31	stroberi	forosadi	+tunda dogo jekundu lililo laini lenye mbegu manjano ndogondogo sana juu ya ngozi yake	
32	sinagogi	hekalu	+jumba la ibada la Wayahudi, mabaniani au mabudha	
33	ikweta	istiwahi	+mstari dhahania unaoizunguka dunia na kuigawa pande mbili zilizo sawa za kasakazini na kusini	
34	protokali	itifaki	+utaratibu maalumu unaotumiwa na maafisa wa serikali katika shughuli rasmi	
35	jaji	hakimu/kadhi	+mtaalamu wa sharia anayesikiliza na kuamua kesi mbalimbali	
36	jeki	gulamu	+mtambo wa kuinulia vitu vizito	
37	piramidi	haram	+jengo la ukumbusho huko Misri lenye msingi wa mraba na ncha kama ya pembe	

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Jumuishi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa
	Kiingereza	Kiarabu		
			tatu lilitumika kuzikia mafarao na wake zao	
38	divisheni	tarafa	+sehemu ya eneo la kiutawala lililo dogo kuliko wilaya lakini kubwa kuliko kata	
39	diploma	stashahada	+cheti maalumu anachopewa mtu ambacho ni chini ya shahada ya kwanza baada ya mafunzo fulani katika chuo	
40	spidi	kasi	+kwa haraka mno +mbio sana	
41	kopi	nakala	+kitu kama maandishi, mchoro au picha kilichonakiliwa	
42	kotiledeni	ghala	+sehemu ya mbegu inayolisha mmea mchanga	

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 3 linaonesha data za utafiti zinazohusisha neno la Kiswahili lenye asili ya Kiingereza na lile la Kiswahili lenye asili ya Kiarabu. Katika data hiyo, maneno yenye asili ya Kiingereza yapo mwanzoni mwa ruwaza kwa sababu mengi miongoni mwa hayo yalibainishwa na watoataarifa walio wengi kuwa yanatumika zaidi kuliko yale yenye asili ya Kiarabu. Mathalani, maneno kama: *digrii, chati, tebo, alfabeti, wiki, sementi, rejesta, risiti, plastiki, namba, bonasi, cheki, propela, divisheni, faili, ikweta, jeki na diploma* yanatumika zaidi kuliko visawe vyake vya shahada, jedwali, abjadi, juma, saruji, sajili, stakabadhi, sandarusi, tarakimu, mukafaa, hawala, daraja, jalada, istiwahi, gulamu na stashahada. Kwa hiyo, wazungumzaji wanapokuwa na maneno mawili yote ya kigeni katika seti ya sinonimu kama *digrii/shahada, chati/jedwali, tebo/jedwali, alfabeti/abjadi, wiki/juma* au *sementi/sarufi* hupendelea kutumia zaidi maneno yenye asili ya Kiingereza kuliko yale yenye asili ya Kiarabu. Hali hii inatokana na matumizi ya lugha ya Kiingereza katika jamii. Lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha rasmi katika nyanja mbalimbali kama vile kufundishia elimu ya sekondari na elimu ya juu. Hivyo, maneno mengi yenye asili ya lugha hiyo ndiyo yanayotumika zaidi ikilinganishwa na yale yenye asili ya Kiarabu. Hata hivyo, suala la uzingativu wa muktadha hutumika kuhitimisha neno lipi litumike zaidi kuliko lingine.

Pamoja na kuwa watoataarifa walio wengi wamebainisha kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiingereza ndiyo yanayotumika zaidi, yapo baadhi ya maneno yenye asili ya Kiarabu yalibainishwa na baadhi ya watoataarifa kuwa yanatumika zaidi kuliko yale yenye asili ya Kiingereza. Mathalani, watoataarifa walibainisha maneno kama *zahanati, tindikali, aya, bara, maradufu, hekalu, itifaki* na *bora* kuwa yanatumika zaidi kuliko visawe vyake vyenye asili ya Kiingereza kama *dispensari, asidi, paragrafu, kontinenti, dabali, sinagogi* na *protokali*. Hivyo, mabadiliko ya

muktadha wa matumizi huweza kuathiri mpangilio wa maneno sambamba na kubainisha neno linalotumika zaidi kuliko lingine.

Ruwaza hizi zina seti nyingi za sinonimu ikilinganishwa na ruwaza zingine. Hali hii inatokana na kuwapo kwa maneno mengi ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza na Kiarabu. Kwa sasa kuna kasi kubwa ya kuingia kwa maneno yenye asili ya Kiingereza katika Kiswahili hasa kwa kuwa kuna maendeleo makubwa katika nyanja za sayansi na teknolojia. Hivyo, istilahi nyingi zimetoholewa kutoka lugha hizo ili kurahisisha kuelezea maarifa mapya yanayogunduliwa kila siku. Kwa upande wa maneno yenye asili ya Kiarabu nayo kuna ongezeko kubwa katika lugha ya Kiswahili kutokana na maarifa ya kidini na mwingiliano mkubwa wa Waswahili na Waarabu.

5.1.3 Ruwaza ya Uwili ya Kiajemi-Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili ya sinonimu za mkopo zinazohusisha maneno yenye asili ya Kiajemi na Kiarabu. Data zilizokusanywa zinaonesha kuwa kuna seti 14 za sinonimu za mkopo zinazohusisha neno la Kiswahili lenye asili ya Kiajemi na lingine lenye asili ya Kiarabu. Maoni ya watoataarifa walio wengi yanaonesha kuwa maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiajemi ndiyo yanayotumika zaidi kwa watumiaji kuliko yale ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Kwa ufafanuzi zaidi hebu tuangalie data za ruwaza hii katika Jedwali Na. 4 lifuatalo:

Jedwali Na. 4: Ruwaza ya Kiajemi-Kiarabu

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiajemi	Kiarabu	
1.	turuhani	bardani	+uzani wa chombo bila ya chochote ndani
2.	turuhani	hadhi	+hali ya kuthaminiwa au kuheshimiwa
3.	staha	adabu/nidhamu	+heshima inayoambatana na haya au aibu ya kutenda lisilo zuri mbele ya watu wengine
4.	dengu	adesi	+mbegu jamii kunde za rangi ya manjano; nafaka za rangi ya manjano zilizo jamii moja na choroko
5.	shaha	kingi	+mfalme katika mchezo wa drafti au sataranji
6.	rangi	launi	+utambulisho wa miale ya nuru katika macho inapoingia katika kitu fulani
7.	boma	faja	+jengo la duara lisilokuwa na paa
8.	dari	sitaha	+sehemu ya mbele au nyuma ya chombo cha baharini ambayo watu hukaa au kuweka mizigo
9.	debwani	rehani	+kitambaa cha hariri chenye mistari myekundu na kahawia ambacho hutumika kwa kazi kama kilemba
10	serikali	dola	+chombo ambacho kwa msingi maalumu kimepewa mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi
11	jambia	hanjari	+silaha ya kisu kipana ambacho huvaliwa kwa

			kupachikwa kwenye nguo tumboni
12	tari	dufu	+ngoma ndogo na nyembamba iliyowambwa upande mmoja na kutiwa vibati kwenye kingo zake
13	nanga	habta	+kitu kizito kinachofungwa na kutoswa majini ili kuzuia chombo kisichukuliwe na maji
14	pilau	kabuli	+wali uliopikwa kwa kuchanganya viungo kama vile mdalasini, iliki pamoja na kitoweo kama nyama na samaki

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 4 hapo juu linaonesha data zinazohusisha ruwaza ya uwili ya Kiajemi-Kiarabu. Katika data hiyo, maneno yenye asili ya Kiajemi yapo mwanzoni kwa sababu yalibainishwa na watoataarifa walio wengi kama maneno wanayoyatumika zaidi ikilinganishwa na visawe vyake vyenye asili ya Kiarabu. Matalani, maneno kama *turuhani, staha, dengu, rangi, boma, dari, debwani, serikali, jambia, tari, nanga* na *pilau* yalibainishwa kama maneno yanayotumika zaidi kuliko visawe vyake vyenye asili ya Kiarabu kama *bardani, nidhamu, adesi, launi, faja, sitaha, rehani, dola, hanjari, dufu, habta* na *kabuli*. Kwa hiyo, panapokuwa na seti ya sinonimu kama *dengu/adesi* au *rangi/launi* watumiaji wa lugha hutumia zaidi neno *dengu* na *rangi* kuliko *adesi* na *launi*.

5.1.4 Ruwaza ya Kiarabu-Kireno

Data za makala haya zimebainisha kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu na Kireno. Kulingana na data zilizokusanywa, imebainika kuwa kuna seti nne za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya uwili ya Kiarabu-Kireno. Maoni ya jumla ya watoataarifa yanaonesha kuwa maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu ndiyo yanayotumika zaidi kuliko visawe vyake vyenye asili ya Kireno. Hivyo, yanakuwa ya kwanza katika ruwaza kama inavyooneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Ruwaza ya Kiarabu-Kireno

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiarabu	Kireno	
1.	deheni	bereu	+mchanganyiko wa grisi, chokaa ambao hupakwa ndani ya jahazi ili lisivunjike
2.	birika/dumu	buli	+chombo cha kutilia chai
3.	mfereji	bomba	+mwanzi mpana na mrefu wa chuma, saruji au plastiki unaopitisha maji au mafuta
4.	shambiro	danguro	+nyumba inayotumiwa kufanyia mambo machafu kama vile umalaya

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Data katika Jedwali Na. 5 zinaonesha sinonimu za mkopo kutoka lugha ya Kiarabu na Kireno. Katika data hiyo, maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu kama *birika* na *mfereji* yamebainishwa kuwa yanatumika zaidi kuliko visawe vyake vya Kiswahili vyenye asili ya Kireno vya *buli* na *bomba*. Hata hivyo, tofauti za kimazingira huweza kusababisha mabadiliko. Kwa mfano, seti ya sinonimu *mfereji/bomba* inatofautiana kimatuzi kutokana na tofauti ya muktadha wa matumizi. Neno *mfereji* hutumika zaidi Tanzania Bara ilhali *bomba* hutumika zaidi Tanzania Visiwani. Hivyo, mfuatano wa maneno katika seti hiyo utabadilika kulingana na eneo la matumizi. Pamoja na maoni ya watoataarifa walio wengi kudai kuwa maneno ya Kiarabu yanatumika zaidi, wapo baadhi ya watoataarifa waliodai kuwa baadhi ya maneno yenye asili ya Kireno kama *danguro* hutumika zaidi kuliko kisawe chake cha *shambilo*, hivyo, kuwa na mabadiliko ya mfuatano wa maneno kwa baadhi ya maneno katika seti.

5.1.5 Ruwaza ya Uwili ya Kiarabu-Kilatini

Data zilizokusanywa na kuchambuliwa zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayohusisha neno la Kiswahili lenye asili ya Kiarabu na lingine lenye asili ya Kilatini. Katika data hiyo, maoni ya watoataarifa wengi yanaonesha kuwa neno la Kiswahili lenye asili Kiarabu ndilo linalotumika zaidi kuliko kisawe chake chenye asili ya Kilatini kama Jedwali Na. 6. linaonyesha kwa muhtasari:

Jedwali Na. 6: Ruwaza ya Kiarabu-Kilatini

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiarabu	Kilatini	
1.	irabu	vokali	+herufi ya alfabeti inayotumika kuwakilisha sauti ambazo si konsonanti

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 6 linaonesha data ya ruwaza ya uwili ya Kiarabu-Kilatini. Katika data hiyo, neno la Kiswahili *irabu* ambalo lina asili ya Kiarabu ndilo linalotumika zaidi kwa watumiaji walio wengi ikilinganishwa na kisawe chake *vokali* ambacho kina asili ya Kilatini. Hali hii ya matumizi ndiyo inayotupatia ruwaza ya uwili ya Kiarabu-Kilatini.

5.1.6 Ruwaza ya Kiingereza-Kihindi

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayohusisha maneno ya Kiswahili yanayotoka lugha ya Kiingereza na Kihindi. Ruwaza hii ina seti nne za sinonimu. Katika ruwaza hii, maoni ya watoataarifa wengi yanaonesha kuwa maneno mengi yenye asili ya Kiingereza ndiyo yanayotumika zaidi kwa watumiaji walio wengi ikilinganishwa na visawe vyake vyenye asili ya lugha ya Kihindi. Data za ruwaza hii zinatolewa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Ruwaza ya Kiingereza-Kihindi

Na.	Asiliya Neno		Kijenzi/Vijenzi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa	Jumuishi
	Kiingereza	Kihindi			
1.	tuktuk	bajaji	+pikipiki ya miguu 3 ya kubebea abiria au mizigo		
2.	feki	bandia	+enye uongo		
3.	boi	chokora	+mwanamume aliyeajiriwa kufanya kazi za nyumbani		
4.	cheki	hundi	+cheti maalumu cha benki kitumikacho kuidhinisha anayetakiwa kupewa fedha		

Chanzo: Data za Uwandani (2021)

Data katika Jedwali Na. 7 zinaonesha seti za sinonimu za ruwaza ya uwili ya Kiingereza-Kihindi. Katika Jedwali hilo, maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza kama *feki*, *boi* na *cheki* yalibainishwa kuwa yanatumika zaidi kuliko visawe vyake vya *bandia*, *chokora* au *cheki*. Hata hivyo, katika seti ya sinonimu *tuktuk* na *bajaji* watoatarifa walibainisha kuwa neno *bajaji* linatumika zaidi kuliko *tuktuk*. Kwa hiyo, kuna mabadiliko ya ruwaza hasa kwa baadhi ya maneno kama seti hiyo inavyoonesha.

5.1.7 Ruwaza ya Kireno-Kihindi

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili ya Kireno-Kihindi. Ruwaza hii ina seti moja ya sinonimu ambayo inahusisha maneno kutoka lugha mbili za kigeni za Kihindi na Kireno. Katika ruwaza hii, maoni ya watoatarifa wengi yanaonesha kuwa neno lenye asili ya Kireno ndilo linalotumika zaidi ikilinganishwa na lile la Kiswahili lenye asili ya Kihindi ambalo halitumiwi sana na watumiaji wengine. Ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii unatolewa kwa muhtasari katika data za Jedwali Na. 8.

Jedwali Na. 8: Ruwaza ya Kireno-Kihindi

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa	Jumuishi
	Kireno	Kihindi			
1.	bibo	kanju	+tunda la mbibo ambalo kokwa yake ni korosho		

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 8 hapo juu linaonesha data zinazohusisha ruwaza ya uwili ya Kireno-Kihindi. Katika ruwaza hiyo, neno *bibo* ambalo lina asili ya Kireno lipo mwanzoni mwa ruwaza kwa sababu ndilo linalotumika zaidi katika jamii ikilinganishwa na neno *kanju* ambalo lina asili ya Kihindi.

5.1.8 Ruwaza ya Kiingereza-Kiajemi

Kulingana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa katika utafiti huu, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayohusisha maneno ya Kiswahili

yenye asili ya Kiingereza na Kiajemi. Ruwaza hii ina seti mbili za sinonimu. Katika ruwaza hii, maoni ya watoataarifa walio wengi yanaonesha kuwa neno moja lenye asili ya Kiingereza ndilo linalotumika zaidi na moja lenye asili ya Kiajemi nalo linatumika zaidi. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame data ya ruwaza hii katika Jedwali Na. 9.

Jedwali Na. 9: Ruwaza ya Kiingereza-Kiajemi

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa	Jumuishi
	Kiingereza	Kiajemi			
1.	yadi	wari	+kipimo cha urefu cha nchi 36 au futi 3		
2.	faksi/telegramu	simu	+matini iliyotumwa kielektroniki		

Chanzo: Data ya Utafiti (2022)

Jedwali Na. 9 linaonesha seti za sinonimu zinazohusisha maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiajemi. Katika seti hizo, neno *yadi* na *faksi* ambayo yana asili ya Kiingereza ndiyo yaliyobainishwa na watoataarifa wengi kuwa yanatumika zaidi kuliko visawe vyake *wari* na *simu*. Hata hivyo, katika data ya *faksi* na *simu* dhana inayorejelewa ndiyo inayosababisha kuwe na mpangilio huo kwa kuwa ni ujumbe na siyo kifaa. Maneno haya ni sinonimu kwa sababu yanahusiana katika dhana iliyobainishwa katika safuwima ya vijenzi jumuishi.

5.1.9 Ruwaza ya Kiingereza-Kireno

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili inayohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na Kireno. Ruwaza hii ina seti moja ya sinonimu ambapo neno lenye asili ya Kiingereza ndilo lililobainishwa na watoataarifa kuwa linatumika zaidi kuliko neno lenye asili ya Kireno. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii, hebu tutazame data hiyo katika Jedwali Na. 10.

Jedwali Na. 10: Ruwaza ya Kiingereza-Kireno

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa	Jumuishi
	Kiingereza	Kireno			
1.	skrubu	parafujo	+msumari wenye hesi		

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 10 linaonesha ruwaza ya sinonimu ya Kiingereza-Kireno. Katika data hiyo, neno *skrubu* ambalo lina asili ya Kiingereza ndilo linalotumiwa zaidi kuliko kisawe chake *parafujo* chenye asili ya Kihindi. Kwa hiyo, neno hilo linakuwa la kwanza katika ruwaza.

5.1.10 Ruwaza ya Kijerumani-Kiingereza

Data za utafiti zimebainisha kuwa Kiswahili kina ruwaza ya uwili ya Kijerumani-Kiingereza. Ruwaza hii inahusisha neno moja la Kiswahili lenye asili ya Kijerumani na lingine lenye asili ya Kiingereza. Katika ruwaza hii, maoni ya watoataarifa

wengi yanaonesha kuwa neno la Kiswahili lenye asili ya Kiingereza ndilo linalotumika zaidi. Hivyo, linakuwa la kwanza katika ruwaza kama Jedwali Na. 11 linavyoonesha.

Jedwali Na. 11: Ruwaza ya Kijerumani-Kiingereza

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kijerumani	Kiingereza	
1.	shule	skuli	+mahali ambapo wanafunzi hufundishwa elimu

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Data katika Jedwali Na. 11 inaonesha ruwaza ya uwili ya Kijerumani-Kiingereza. Neno *shule* ambalo lina asili ya Kijerumani ndilo linalotumika zaidi kuliko kisawe chake *skuli* ambacho kina asili ya Kiingereza. Hata hivyo, suala la utumizi wa maneno haya ni wa kimaeneo zaidi. Kwa hiyo, mfuatano wake huweza kubadilika kulingana na eneo/muktadha wa matumizi. Kwa mfano, neno *shule* linatumika zaidi Tanzania Bara ilhali neno *skuli* linatumika zaidi Tanzania Visiwani. Hivyo, katika muktadha wa Tanzania Visiwani ni dhahiri kuwa neno *skuli* litabainishwa kuwa linatumika zaidi kuliko kisawe chake *shule* ambacho kinatumika zaidi Tanzania Bara.

5.1.11 Ruwaza ya Kiingereza-Kifaransa

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya uwili ya Kiingereza-Kifaransa. Ruwaza hii inahusisha neno la Kiswahili lenye asili ya Kiingereza na lingine lenye asili ya Kifaransa. Katika ruwaza hiyo, maoni ya watoataarifa walio wengi yanaonesha kuwa neno moja lenye asili ya Kiingereza linatumika zaidi kuliko kisawe chake chenye asili ya Kifaransa na neno lingine lenye asili ya Kifaransa nalo linatumika zaidi kuliko kisawe chake chenye asili ya Kiingereza. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii tutazame data katika Jedwali Na. 12.

Jedwali Na. 12: Ruwaza ya Kiingereza-Kifaransa

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiingereza	Kifaransa	
1.	vanila	lavani	+kiungo ambacho kinatokana na mvanila kinachotumiwa katika chakula ili kuleta harufu nzuri
2.	kamisi	shimizi	+vazi refu la ndani +wanawake

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 12 linaonesha seti za sinonimu zinazohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na Kifaransa. Katika data hiyo, neno *vanila* lenye asili ya Kiingereza ndilo linalotumika zaidi kuliko kisawe chake *lavani* huku neno *shimizi*

lenye asili ya Kifaransa nalo linatumika zaidi kuliko kisawe chake *kamisi*. Kwa hiyo, katika ruwaza hii utumizi wa maneno ni wa asilimia 50 kwa 50. Hivyo, kuna mabadiliko ya matumizi ya maneno kutokana na muktadha wa matumizi. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame aina nyingine ya ruwaza katika kipengele kinachofuata.

5.1.12 Ruwaza ya Kifaransa-Kireno

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya sinonimu inayohusisha neno moja kutoka Kifaransa na lingine kutoka Kireno. Ruwaza hii ina seti moja ya sinonimu. Katika ruwaza hii, maoni ya watoataarifa walio wengi yanaonesha kuwa neno la Kiswahili lenye asili ya Kifaransa ndilo linalotumika zaidi kuliko lile lenye asili ya Kireno kama Jedwali Na. 13 linavyoonesha.

Jedwali Na. 13: Ruwaza ya Kifaransa-Kireno

Na.	Asili ya Neno		Kijenzi/Vijenzi (TUKI, 2019)	Maana/Fahiwa	Jumuishi
	Kifaransa	Kireno			
1.	divai	mvinyo	+kileo kinachotengenezwa kwa maji ya zabibu		

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Jedwali Na. 13 linaonesha data inayohusisha ruwaza ya uwili ya Kifaransa-Kireno. Katika data hiyo, neno lenye matumizi zaidi ni *divai* kuliko kisawe chake *mvinyo*. Hivyo, neno hilo linakuwa mwanzoni mwa ruwaza. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa baadhi ya seti za sinonimu kubadilika kulingana na muktadha, seti hii pia hubadilika kulingana na muktadha wa matumizi. Kuna baadhi ya miktadha neno *mvinyo* hutumika zaidi kuliko *divai*.

5.2 Ruwaza ya Utatu wa Sinonimu

Ruwaza ya utatu wa sinonimu inahusisha maneno matatu kutoka lugha tatu tofauti. Utafiti huu umebaini kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu wa sinonimu. Hata hivyo, tofauti na seti za ruwaza ya uwili, ruwaza ya utatu haina seti nyingi za sinonimu. Ndani ya ruwaza hii ya utatu kuna ruwaza ndogondogo zinazojitokeza. Ruwaza zilizobainika ni pamoja na ruwaza ya Kiingereza/Kihindi/Kiarabu na ruwaza ya Kiajemi-Kiarabu-Kihindi. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hizi, tutazame data katika Jedwali Na. 14 na Jedwali Na. Na. 15.

Jedwali Na. 14: Ruwaza ya Kiingereza-Kihindi-Kiarabu

Na.	Asili ya Neno			Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiingereza	Kihindi	Kiarabu	
1.	cheki	hundi	hawala	+cheti maalumu cha benki kitumikacho kuidhinisha anayetakiwa kupewa fedha

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Data katika Jedwali Na. 14 zinaonesha seti ya sinonimu inayohusisha maneno kutoka lugha tatu ambazo ni Kiingereza-Kihindi-Kiarabu. Katika ruwaza hiyo, neno la Kiswahili *cheki* ambalo lina asili ya Kiingereza ndilo lililobainishwa na watoataarifa kama neno linalotumika zaidi ikilinganishwa na visawe vyake vya *hundi* na *hawala*. Hivyo, neno hilo linakuwa la kwanza katika ruwaza. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii ya utatu wa sinonimu, tutazame ruwaza nyingine ya utatu katika Jedwali Na. 15.

Jedwali Na. 15: Ruwaza ya Kiajemi-Kiarabu-Kihindi

Na.	Asili ya Neno			Kijenzi/Vijenzi Maana/Fahiwa Jumuishi (TUKI, 2019)
	Kiajemi	Kiarabu	Kihindi	
1.	pilau	kabuli	kubuli	+wali uliopikwa kwa kuchanganya viungo kama vile mdalasini, iliki, pamoja na kitoweo kama nyama na samaki

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Data katika Jedwali Na. 15 zinaonesha seti ya sinonimu inayohusisha maneno ya Kiswahili yanayotoka lugha ngeni tatu ambazo ni Kiajemi, Kiarabu na Kihindi. Katika data hiyo, maoni ya watoataarifa walio wengi yanaonesha kuwa neno *pilau* ambalo lina asili ya Kiajemi ndilo linalotumika zaidi kwa wanajamii walio wengi kuliko visawe vyake *kabuli* kutoka Kiarabu na *kubuli* kutoka Kihindi.

6.0 Hitimisho

Kwa ujumla, makala haya yamebainisha ruwaza mbalimbali zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo katika lugha ya Kiswahili. Ruwaza zilizobainika ni ya uwili na utatu wa sinonimu. Ruwaza ya uwili inahusisha maneno kutoka lugha mbili za kigeni na ruwaza ya utatu inahusisha maneno kutoka lugha ngeni tatu. Matokeo haya yanatofautiana na Kitundu (2022) ambaye alipata ruwaza nne za sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwapo kwa ruwaza mbili za sinonimu za mkopo. Kati ya ruwaza zilizobainika, ruwaza ya uwili ndiyo inayojitokeza zaidi ikilinganishwa na ruwaza ya utatu. Suala la kuwapo kwa ruwaza nyingi za uwili liliwahi pia kubainishwa na watafiti tangulizi kama Kitundu (2022) ambaye alibaini kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza nyingi za uwili kuliko za utatu, unne na utano. Kuwapo kwa ruwaza hizi kunatokana na kuwapo kwa maneno ya mkopo katika lugha ya Kiswahili kutoka lugha kama Kiingereza, Kihindi, Kihispaniola, Kiajemi, Kiarabu, Kireno na Kijerumani. Ukopaji unaoibua ruwaza hizi kama ilivyowahi kuelezwa na Kiango (1999), unatokana na kasumba ya wazungumzaji kukopa maneno pindi wanapotagusana na jamii ngeni hata kama neno linalorejelea dhana hiyohiyo lilikwisha kukopwa kutoka lugha nyingine ya kigeni. Hata hivyo, data zinaonesha kuwa maneno mengi ya Kiswahili yametoholewa kutoka lugha ya Kiingereza na Kiarabu ikilinganishwa na lugha kama Kijerumani, Kireno, Kifaransa, Kilatini, Kiajemi au Kihindi. Hivyo, ruwaza nyingi zimehusisha maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Katika ruwaza

hizo, mfuatano wa maneno unabadilika kulingana na lugha zinazohusika pamoja na muktadha wa matumizi. Haya yaliwahi pia kubainishwa na Ullmann (1967) na Kitundu (2022) kuwa ruwaza huweza kubadilika kulingana na sababu mbalimbali mojawapo ikiwa ni mabadiliko katika muktadha wa matumizi. Hivyo, baadhi ya maneno katika seti yanaweza kutumika zaidi katika muktadha fulani kuliko maneno mengine katika seti hiyohiyo ambayo nayo huweza kutumika katika muktadha fulani kuliko maneno mengine. Hali hii huathiri ruwaza kimfuatano. Makala haya yanahitimisha kuwa ukopaji wa maneno kutoka lugha ngeni mbili au zaidi huibua sinonimu za mkopo ambazo kimatumizi huwa na ruwaza fulani. Ruwaza hizo hubadilika kulingana na mabadiliko ya muktadha wa kimatumizi.

Marejeleo

- Celeghin, D. (2013) *Different Forms, Different Meaning? A Lexicographic and Corpus-Based Study of Four Sets of English Near-Synonyms*. Tasinifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Degli Stud di Dadova, Dedli. Inapatikana katika <https://thesis.unipd.it/handle/20.500.12608/17701>. Ilisomwa Tarehe 30 Septemba 2022.
- Chacha, L. M. na Malangwa, P. S. (2019) *Semantiki*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Chuwa, A. R. (1988) "Foreign Loan Words in Kiswahili". *Kiswahili*. Juz. Na. 55(1) na 55(2): 163-172.
- Cruse, A. (2006) *A Glossary of Semantics and Pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Danglli, L. (2010) "Origin of Synonyms and their Acquisition as Vocabulary". *LCPJ Publishing*, Juz. Na. 3(2): 66-72. Inapatikana katika [https://www.lcpj.pro/skedaret/1355270481-Revista%20LCPJ 3 2 31.pdf](https://www.lcpj.pro/skedaret/1355270481-Revista%20LCPJ%203%202010.pdf). Ilisomwa Tarehe 20 Septemba 2022.
- Geeraerts, D. (2009) *Theories of Lexical Semantics*. New York: Oxford University Press.
- Grey, L. H. (1964) *Foundations of Language*. New York: The Macmillan Company.
- Griffiths, P. (2006) *An Introduction to English and Pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hoffer, B. L. (2005) "Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity". *Intercultural Communication Studies*, Juz. 14(2): 53-72. Inapatikana katika <https://web.uri.edu/iaics/files/05-Bates-L.-Hoffer.pdf>. Ilisomwa tarehe 15 Septemba 2022.
- Kahigi, K. K. (2019) *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

- Kiango, J. G. (1999) "Matatizo ya Utohozi wa Maneno kama Mbinu ya Kukopa Istilahi katika Lugha". *Mulika*, Juz. 25: 1-8.
- King'ei, K. (2010) *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kreidler, C. W. (1998) *Introducing English Semantics*. London: Routledge.
- Kitundu, G. J. (2022) *Ruwaza Zinazojitokeza kwenye Sinonimu za Asili na za Mkopo katika Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B. (2009) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matinde, R. S. (2012) *Dafina ya Lugha*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.
- Mohamed, M. (2010) *A Study of Adaptation of Arabic Loanwords in Swahili Dictionary: A Case of Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI 2004). Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mohamed, M. A. na Mohamed, S. A. (2014) *Kamusi ya Visawe*. Royapettah: Rathna Offset Printers.
- Ndimele, O. (1997) *Semantics and the Frontiers of Communication*. Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Ltd.
- Palmer, F. R. (1976) *Semantics* (Toleo la 2). Cambridge: Cambridge University Press. .
- Resani, M. (2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Print Technology.
- Robins, R. H. (1980) *General Linguistics*. London: Lonmans.
- Shembilu, M. M. (2017) *Michakato ya Kisemantiki kwenye Maneno ya Mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka Kiingereza na Kiarabu*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Skallman, E. (2012) *The Interplay of Synonymy and Polysemy: The Case of Arrojar, Echar, Ianzar and Tirar*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tromso, Toronto. Inapatikana katika <https://munin.uit.no/bitstream/handle/10037/4395/thesis.pdf?sequence=2&isAllowed=y>. Iisomwa tarehe 28 Septemba 2022.
- TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: OUP.
- Ullmann, S. (1967) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford.
- Wittgenstein, L. (1953) *Philosophical Investigations*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.
- Zhou, Li. (2016) "Loan Words in Modern English and Their Features". *Sino-US English Teaching*, Juz. 13(3): 209-212.